

UNYANYASAJI WA WANYAMA

Na Augustino Chengula

Unyanyasaji/utesaji wa wa wanyama umekuwa ukifanywa katika maeneo mengi ya nchi tangu kuanza kwa ufugaji ikiwa ni pamoja na kuwaburuta wanyama kwa viboko hadi kupelekea ngozi ya miili yao kuchubuka, kuwa na vidonda na wengine hata kupoteza uhai. Wafugaji wengine wamekuwa wakiwakata mikia mifugo wao, wakiwachoma kwa vitu vyenye ncha kali au moto, kuwatoa pembe kwa kuwapiga na vitu vizo kama virungu, mawe n.k. Ng'ombe wengine wamepata ufu wa macho kwa kupigwa na mwanadamu na wengine wamevunjwa mguu mmoja au zaidi. Haya ni baadhi tu ya mateso wanayopewa wanyama wanaofugwa na binadamu kwa manufaa yake. Ipo mifano mingi ya manyanyaso kwa mifugo yetu yanayofanywa na wafugaji na wasio wafugaji. Si kwamba hatufahamu kuwa wanyama nao wanapta maumivu kama wanadamu la hasha tunafahamu sana. Tatizo nini, ni ubabe tu wa mwanadamu wa kutaka kuwa na madaraka juu vitu, wanyama au mwanadamu mwenzake. Ndoo maana tunaona kuwa mwanadmu akimnyanyasa mwenzake na sheria zikitungwa kuweka mambo sawa. Tanzania kuona kadhia hii ya wanyama kuititia bunge lake lilitunga na kuitisha sheria ya ustawi wa wanyama ya mwaka 2008 inayopatikana [hapa](#). Sheria hii inazuia unyanyasaji wa wanyama unaofanywa na binadamu, kwenda kinyume nayo ni makosa makubwa na ukibainika sheria lazima ifuate mkondo wake. Tushirikiane kuhakikisha tunawaelimisha wananchi wote wenye mifugo na wasio nayo ili waone umuhimu wa kuthamini mifugo inayowaletea faida nyingi na maendeleo kwa taifa letu.



Hii ni picha kutoka mkoa wa Morogoro. Tumezoea kuona mishikati ya binadamu tu,
lakini hapa tunaona na ng'ombe akiwa sehemu ya mshikaki